

Mwongozo wa Kozi. Nyaraka za Agano Jipya

Kitabu cha Waebrania

Kitabu cha Yakobo

Kitabu cha Ufunuo

MAELEKEZO YA KOZI

Kozi hii inaelezea historia ya awali, madhumuni, muundo na yaliyomo katika Waebrania, Yakobo, na ufunuo, vitabu vitatu vya Agano Jipya vyenye changamoto, matukio na vyenye muundo wa kushangaza. Madhumini na Mada nyingi za vitabu hivi ni ngumu kuzielewa, lakini inatupa ufahamu kuwa hadhira yao ya awali ilikuwa ikikabiliwa na mateso na kwamba walijaribiwa kiasi cha kutaka kumkana Kristo. Kozi hii ina mfululizo wa video za Thirdmill, Kitabu cha Waebrania, Waraka wa Yakobo na Kitabu cha Ufunuo, vimetolewa na Third Millennium Ministries na kuwasilishwa na Dkt. Stephen Um, Dkt. Paul Gardner, akishirikiana na Dkt. Steve Brown, na maprofesa mbalimbali wamehusika katika kukamilisha kozi hii.

MALENGO NA MALENGO MAHUSUSI

Malengo

Katika kozi hii tunategemea utatimiza yafuatayo:

1. Tunatumaini kuwa utatumia nyenzo zote za kozi kujifunza mambo muhimu kuhusu historia ya awali, madhumuni, muundo na maudhui ya Waebrania, Yakobo na Ufunuo, ukijibu maswali kama vile:
 - Nani aliyeandika, na kwa nini?
 - Malengo makuu ya vitabu ni yapi?
 - Tunapaswa kuzitumia kwa namna gani mada za vitabu hivi?
2. Tunatumaini utatiwa moyo katika maisha yako ya Kikristo na kukua katika ufahamu wako kupitia hekima zinazopatikana katika vitabu hivi vitatu.
3. Tunatumaini utafanya mabadiliko katika maisha yako, kupitia mafundisho ya nyaraka hizi tatu za Agano Jipya, hasa ukishiriki katika kuwasaidia Wakristo wanaokabiliwa na mafundisho ya uongo, mafundisho yenye upumbavu, na wanaokata tamaa kutokana na majaribu wakitaka kuiacha Imani.

Malengo Mahususi

Ukishafanya haya itaonyesha kuwa malengo mahususi yamefikiwa:

1. Pata alama za kuridhisha kwenye maswali na mitihani, itaonyesha kwamba unaweza kutambua taarifa muhimu kuhusu historia ya awali, madhumuni, muundo na maudhui ya nyaraka hizi.
2. Kamilisha miongozo ya somo na kazi zinazohusiana na beji ya kozi, ukielezea mtazamo na mawazo yako kuhusu mafundisho ya barua hizi. Kisha yatumie mawazo hayo katika huduma na maisha yako
3. Shiriki katika mijadala ya kila wiki kagua na kutafakari juu ya mafundisho ya video za Thirdmill, ili kuzielewa kikamilifu dhana na kuzitumia katika maisha na huduma yako.

Orodha ya Moduli za Kozi ya Nyaraka za Agano Jipya

1. Waebrania: Historia ya awali na kusudi
2. Waebrania: Muundo na Maudhui
3. Yakobo: Utangulizi
4. Yakobo: Hekima ya namna mbili
5. Ufunuo: Historia ya Awali
6. Ufunuo: Muundo na Maudhui: sehemu ya kwanza
7. Ufunuo: Muundo na Maudhui: sehemu ya pili
8. Ufunuo: Mfalme na Ufalme wake

VIPENGELE VYA KOZI

Beji

1. Kila wiki ya Majadiliano katika kundi, tenga muda kwa ajili ya kufanya kazi pamoja na hati ya beji. Mwongozo huu wa kurasa mbili utatoa mwelekeo wa jumla kwa mkufunzi wako unapotafuta kukuza ujuzi huu muhimu wa huduma.
2. Katika wiki chache, sehemu ya muda wako wa majadiliano itatumika kupitia Mada za majadiliano zilizotolewa katika maagizo ya beji.
3. Ukiisha kuwa na msingi mzuri wa majadiliano ya kikundi tumia wiki zilizobaki kufanya kazi ya Beji ya ***Wito kwa vitendo***.
4. Utatunukiwa beji endapo Mkufunzi wako atakaporidhika kuwa umekamilisha hatua, kwa kuzingatia maelekezo ya hatua za vitendo za Beji.

Moduli

1. Soma masomo, na kutazama **video**, sikiliza **sauti**, au Soma **nukuu za somo**.
2. Kamilisha **Miongozo ya Somo** kwa kila Moduli. Tumia Miongozo ya masomo kujitayarisha kwa ajili ya **maswali ya mtandaoni**.
3. Fanya majaribio kwa njia ya mtandao kwa kila moduli. Unaweza kufanya Majaribio mara nyingi kwa kadri uwezavyo, lakini itakupasa kusubiri saa moja kabla ya kurudia jaribio hilo. Alama za juu utakazopata katika jaribio zitatumika rasmi. Tunashauri upate angalau

80% kabla ya kushiriki katika majadiliano ya kila wiki ili kuhakikisha kuwa unaelewa dhana kwa usahihi.

4. Shirikiana na kundi lako katika *majadiliano* ya kila wiki, pamoja na mkufunzi wako, kwa kutumia ***Mwongozo wa majadiliano***. Majadiliano ni muhimu kwa ajili ya kukuza ufahamu wako wa matumizi ya nyenzo za kozi, lakini pia yanakuza uwezo wako wa kutumia dhana kwa usahihi katika maisha na huduma yako. Tunapoendelea mjadala wa kila moduli udumu angalau kwa saa moja.

Mtihani wa Mwisho

Unaweza kufanya mitihani mara nyingi kama uwezavyo, lakini ni lazima usubiri saa moja kwa kila mtihani. Daraja lenye alama za juu, ndilo litachukuliwa kuwa rasimi, ni lazima ufikie 80% kwenye mtihani wa mwisho.

MADARAJA

Daraja la Mtihani wa mwisho linahesabiwa kama ifuatavyo:

1. Maswali kwenye hotuba yana thamani ya alama 30.
2. Mtihani wa mwisho una thamani ya 100.
3. Beji haitaathiri daraja lako, lakini lazima ikamilishwe na kuridhiwa na mkufunzi na iwekwe kwenye alama kuwa imekamilika katika orodha ya uhakiki wa mafunzo ya Biblia.

Ufaulu wa juu ni kuanzia 80%

Orodha ya walioshiriki kuandaa kozi:

Dkt. Jimmy Agan ni profesa mshiriki wa Agano Jipya na mkurugenzi wa Homiletics katika Seminari ya Kitheolojia ya Agano.

Mch. Ivan Bepalov ni Mchungaji wa Kanisa la Utatu Mtakatifu huko Kiev, Ukraine.

Dkt. Steve Blakemore ni profesa Msaidizi wa Falsafa katika Seminari ya Wesley Biblical Seminary.

Dkt. Constantine R. Campbell ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya katika Shule ya Trinity Evangelical Divinity School.

Dkt. D.A. Carson ni Profesa Mtafiti wa Agano Jipya katika shule ya Trinity Evangelical Divinity School na Mwanzilishi Mwenza wa Gospel Coalition.

Dkt. David W. Chapman ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya na Akiolojia katika Seminari ya Covenant Theological Seminary.

Dkt. Robert B. Chisholm, Jr. ni Mwenyekiti wa Idara ya Agano Jipya katika Seminari ya Dallas Theological Seminary.

Dkt. Brandon D. Crowe ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya katika Seminari ya Westminster Theological Seminary.

Dkt. Dan Doriani ni Makamu wa Raisi wa Mradi wa Kimkakati wa Kitaaluma na Profesa wa Theolojia katika Seminari ya Theolojia ya Agano.

Bw. Steve Douglass ni Raisi na Mwenyekiti wa bodi ya Timu ya Campus Crusade for Christ International.

Dkt. William Edgar Profesa wa Apologetics katika Seminari ya Theolojia ya Westminster.

Dkt. Matt Friedeman ni Profesa wa Uinjilisti na Ufuasi katika Seminari ya Wesley Biblical Seminary.

Dkt. David B. Garner ni Profesa Mshiriki wa Theolojia ya Utaratibu katika Seminari ya Theolojia Westminster huko Glenside, Pennsylvania.

Dkt. Jeffrey A. Gibbs ni Profesa wa Theolojia ya Ufafanuzi katika Seminari ya Concordia.

Dkt. Benjamin Gladd ni Profesa Msaidizi wa Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia iliyorekebisha.

Mch. Michael J. Glodo ni Profesa Mshiriki wa Masomo ya Biblia katika Seminari ya Theolojia iliyorekebisha huko Orlando, Florida.

Dkt. James M. Hamilton ni Profesa wa Theolojia ya Biblia katika Seminari ya Southern Baptist Theological na Mchungaji na Mhubiri katika Kanisa la Baptisti la Kenwood.

Dkt. Dennis E. Johnson ni mtaaluma mkuu na Profesa wa Theolojia ya Vitendo katika Seminari ya Theolojia inayoitwa Westminster huko California.

Bw. Bradley T. Johnson ni Mchungaji katika kanisa la Methodisti na Profesa katika Seminari ya Theolojia ya Asbury.

Dkt. Barry Joslin ni Profesa mshiriki wa theolojia ya Kikristo na mratibu wa mkakati wa Masomo ya Theolojia ya Kikristo katika chuo cha Boyce huko Louisville, Kentucky.

Dkt. Edward M. Keazirian ni Profesa msaidizi wa Mkakati wa lugha ya Kigiriki katika Seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.

Dkt. Thomas L. Keene ni Mchungaji Mshiriki wa Huduma za Kifamilia katika Kanisa la Kristo Mfalme la Presbyterian na Mhadhiri wa Muda katika Seminari ya Theolojia ya Westminster huko Glenside, PA.

Dkt. Craig S. Keener ni F.M. na Mwenyekiti wa Ada Thompson ya Masomo ya Biblia katika Seminari ya Theolojia inayoitwa Asbury.

Dkt. Michael Kennison ni Mchungaji Mshiriki wa Kirk of the Hills huko St. Louis, MO.

Dkt. Simon J. Kistemaker ni Profesa mstaafu wa Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia iliyorekebisha huko Orlando, Florida.

Mch. David Lewis ni Profesa Msaidizi Theolojia ya Ufafanuzi katika Seminari ya Concordia.

Dkt. Robert G. Lister ni Profesa wa Biblia na Masomo ya Theolojia katika Shule ya Theolojia inayoitwa Talbot.

Dkt. Fredrick Long ni Profesa wa Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia ya Asbury.

Dkt. Dan McCartney alikuwa Profesa wa Fafanuzi za Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia inayoitwa Redeemer.

Dkt. Sean McDonough ni Profesa wa Agano Jipya katika Seminari ya Theolojia inayoitwa Gordon-Conwell.

Dkt. John E. McKinley ni Profesa wa Biblia na Masomo ya Theolojia katika Shule ya Theolojia ya Talbot.

Dkt. Thomas J. Nettles ni Profesa wa Historia ya Theolojia katika Seminari ya Theolojia inayoitwa Southern Baptist.

Dkt. John Oswalt ni Profesa Mashuhuri wa Agano la Kale katika Seminari ya Theolojia inayoitwa Asbury.

Dkt. Alvin Padilla ni Makamu Raisi wa Maswala ya Taaluma katika Seminari ya Western Theological Seminary.

Dkt. Greg Perry ni Makam Raisi wa Kimkakati wa Miradi katika Huduma ya Third Millennium Awali alikuwa Profesa Mshiriki wa Agano Jipya na Mkurugenzi wa huduma ya Mipango katika Seminari inayoitwa Covenant Theological.

Dkt. Vern S. Poythress ni Profesa wa Fafanuzi za Agano Jipya katika Seminari ya Westminster Theological Seminary na Mhariri wa Makala ya Kitheolojia ya Westminster.

Dkt. Richard L. Pratt, Jr. ni Mwanzilishi Mwenza na Raisi wa Huduma ya Third Millennium.

Dkt. Scott Redd ni Raisi wa Kampasi ya Seminari ya Theolojia iliyorekebisha huko Washington D.C. na Profesa wa Agano la Kale.

Dkt. Eckhard Schnabel ni Mary F. Rockefeller Profesa aliyebobea katika Masomo ya Agano Jipya katika Seminari ya Gordon-Conwell.

Dkt. Thomas R. Schreiner ni profesa wa James Buchanan Harrison anahusika na Tafsiri za Agano Jipya na Mtaaluma Mshiriki katika Maandiko na Fafanuzi katika Seminari itwayo Southern Baptist Theological Seminary.

Dkt. Glen Scorgie ni Profesa wa Theoloji katika Seminary ya Bethel, huko San Diego.

Dkt. James D. Smith III ni Profesa Mshiriki wa Historia ya Kanisa katika Seminari ya Bethel, San Diego, na Profesa wa Dini katika Chuo Kikuu cha San Diego.

Dkt. Mark L. Strauss ni Profesa wa Agano Jipya katika Seminari ya Bethel, huko San Diego.

Dkt. K. Erik Thoennes ni Profesa wa Biblia na Masomo ya Theolojia katika chuo kikuu cha Shule ya Theolojia kiitwacho Biola University's Talbot na Mwenyekiti wa Idara ya Biblia na Masomo ya Theolojia.

Mch. Dkt. Stephen Tong ni Mwinjilisti mashuhuri wa China na Mwanatheolojia, mwanaharakati wa mageuzi ya Kiinjili na Mwanzilishi wa Huduma ya Tong Evangelistics (STEMI) na profesa wa Seminari ya Reformed Evangelical Church huko Indonesia.

Dkt. Carl R. Trueman ni Profesa wa Historia ya Theolojia na Historia ya Kanisa, pia ni Mwenyekiti wa Historia ya Paul Woolley katika Seminari ya Westminster Theological huko Glenside, Pennsylvania.

Dkt. William Ury ni Profesa wa Theolojia na historia ya Theolojia katika Seminari inayoitwa Wesley Biblical Seminary.

Dkt. Miles Van Pelt ni Profesa wa Agano la Kale na Mtaaluma mkuu katika Seminari ya Theolojia iliyorekebisha.

Dkt. Simon Vibert alikuwa Kasisi wa Kanisa la Mtakatifu Luka huko Wimbledon Park, UK, na kwa sasa ni Makamu Mkuu wa Wycliffe Hall, Oxford, na Mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri.

Dkt. Peter Walker ni Profesa wa Masomo ya Biblia katika Shule ya Huduma inayitwa Trinity na hapo awali alikuwa Mhadhiri wa Masomo ya Biblia na Makamu mkuu wa chuo cha Oxford, Wycliffe Hall.

Mch. Dkt. Michael Walker Mwanatheolojia katika Kanisa la Highland Park Presbyterian huko Dallas, TX.

Dkt. Larry J. Waters ni Profesa wa Fasiri za Biblia Seminari ya Theolojia inayoitwa Dallas Theological Seminary.

Dkt. Stephen J. Wellum ni Profesa wa Theolojia ya Kikristo katika Seminari ya Southern Baptist Theological.

Mch. Dkt. Thurman Williams ni Mchungaji Mshiriki katika Ushirika uitwao Neema na Amani huko St. Louis, MO.

D

kt. Ben Witherington III ni Profesa wa Tafsiri za Agano Jipya katika Seminari inayoitwa Asbury Theological Seminary.

Dkt. Stephen E. Witmer ni profesa wa Viambatanisho vya Agano Jipya katika seminari ya Gordon-Conwell na Mchungaji Kiongozi wa Ushirika wa Pepperell Christian Fellowship huko Pepperell, MA.